

# Sensa ya Marekani mwaka 2020

## Kile unachopaswa kujua

### Sensa ya Marekani ni nini?

Mara moja kila baada ya miaka 10, serikali ya Marekani inajaribu kumhesabu kila mtu katika nchi hiyo kulingana na wanakoishi. Hii inaitwa Sensa.

Sheria inahitaji kila mtu anayeishi Marekani (*bile kujali hadhi ya uhamiaji*) kujibu. Ikiwa uliwasili Marekani baada ya **Aprili 1, 2020**, huhitaji kujibu.

Serikali haishiriki habari zako binafsi na mtu yeyote, hata watu wengine serikalini au polisi. Hiyo ni kinyume cha sheria.

### Kwa nini ni muhimu?

Idadi ya watu wanaohesabiwa wanaathiri fedha za serikali kwa ajili ya shule, hospitali, usafirishaji, na makazi katika jamii yetu, na vilevile ajira na programu unazotumia. Kutoa habari yako itasaidia rasilimali za jamii na mipango inayosaidia familia yako na watoto.

### Unapaswa kutarajia nini?

Fomu hiyo ni fupi. Serikali ya Marekani inauliza juu ya idadi ya watu wanaoishi katika anwani yako, ikiwa unamiliki au unakodisha nyumba yako, na nambari yako ya simu. Kwa kila mtu anayeishi nyumbani kwako, serikali inauliza jina lake, ni mara ngapi wanaishi hapo, uhusiano wa mtu huyo na wewe, ikiwa ni wa kiume au wa kike, umri wake, tarehe yake ya kuzaliwa, na kabila lake. Hii ni pamoja na watoto wako. Wewe **HUTAULIZWA** kuhusu nambari yako ya hifadhi ya jamii au habari zozote kuhusu fedha.

### Unaulizwa ufanye nini?

Mnamo Machi utapokea barua katika sanduku la barua la nyumbani kwako ikikuomba utoe habari juu ya nani anayeishi hapo. Unaweza kutoa habari yako kwenye karatasi unayoipokea, kwenye kompyuta au simu yako, au kwa kupiga simu. Ikiwa hautajibu katika moja ya njia hizi, utakuwa na fursa nyingine: mtu kutoka serikali ya Marekani anaweza kuja nyumbani kwako na kukuomba ujibu ana kwa ana.

Wasiliana na

ukiwa na maswali yoyote.

